# MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI (CMT) KILICHOFANYIKA TAREHE 24 FEBRUARI, 2022

| WALIOHUDHURIA | WAJUMBE | |
|---|---|---|
| 1. Dr. Omary A. Nnkullo | Mkurugenzi Mtendaji (W) | M/Kiti |
| 2. Ndg. Salum S. Dhamin | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango | Katibu |
| 3. Ndg. Unamwe Erasto | Kaimu Mkuu wa Kitenbgo cha Uchaguzi | Mjumbe |
| 4. Ndg. Nkinde M. Mwaikuka | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA | Mjumbe |
| 5. Ndg. Sudi Abdul | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari | Mjumbe |
| 6. CPA Jacqueline J. Kigwa | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Mjumbe |
| 7. Ndg. Geofrey G. Kalatunga | Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Kongwa | Mjumbe |
| 8. Ndg. Foska E. Mgovano | Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Kibaigwa | Mjumbe |
| 9. Ndg. Msafiri V. Mkunda | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | Mjumbe |
| 10. Mhs. David I. Chitemo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo | Mjumbe |
| 11. Ndg. Eugen Shirima | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi | Mjumbe |
| 12. Dr. Thomas N. Samweli | Mkuu wa Idara ya Afya | Mjumbe |
| 13. Ndg. Hamisi Y. Sombwe | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili | Mjumbe |
| 14. Mhs. Anitha K. Muhula | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi | Mjumbe |
| 15. Ndg. Elias J. Chilemu | Mratibu wa TASAF (W) | Mjumbe |
| 16. Ndg. Mugeta M. Kurwijira | Mratibu wa Mfuko wa Elimu (W) | Mjumbe |

## SEKRETARIETI

| | |
|---|---|
| Ndg. Emmanuel C. Thobias | Mwandishi wa Vikao (CC) |
| Ndg. Credo B. Kanyabuhura | Mwandishi wa Vikao (CC) |

## CMT/KOG/2021-22/05/01: KUFUNGUA KIKAO.

Kabla ya kufungua kikao wajumbe walisali sala ya Menejimenti. Baada ya sala hiyo, Mwenyekiti alikaribishwa kwa ajili ya kufungua kikao ambapo pamoja na masuala mengine aliwasihi wajumbe kushiriki kikao kikamilifu. Aidha, aliwataarifu kuwa kikao hicho ni kwa ajili ya kujadili taarifa za mwezi Januari, 2022 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Baada ya utangulizi huo, Mwenyekiti alifungua kikao saa 5:52 asubuhi.

## CMT/KOG/2021-22/05/02: KUPOKEA NA KUTHIBITISHA AJENDA ZA KIKAO.

Jumla ya ajenda tisa (9) zilipokelewa na kuthibitishwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kupokea na kuthibitisha ajenda za kikao.
3. Kusoma, kuthibitisha muhtasari na kupitia yatokanayo na kikao cha Menejimenti cha tarehe 28/01/2022.
4. Kusoma muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 09/02/2022 na kupitia yatokanayo na kikao hicho.
5. Taarifa za Mapato na matumizi ya Halmashauri
   a) Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Halmashauri kwa mwezi Januari, 2021
   b) Taarifa ya mapato na matumizi katika vituo vya kutolea huduma za afya mwezi Januari, 2022
6. Taarifa ya makusanyo ya mfuko wa Elimu kwa mwezi Januari, 2022.
7. Hoja ya uendeshaji wa machinjio ya kuku, kiwanda cha maziwa na bwawa la ufugaji wa samaki



Scanned with CamScanner

8. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19 kwa Idara za Afya, Elimu msingi na Sekondari.
9. Kufunga kikao.

## CMT/KOG/2021-22/05/03: KUSOMA, KUTHIBITISHA MUHTASARI NA KUPOKEA YATOKANAYO NA KIKAO CHA MENEJIMENTI CHA TAREHE 28 JANUARI, 2022.

Wajumbe walipata fursa ya kusoma muhtasari wa kikao cha Menejimenti cha tarehe 28 Januari, 2022 na kuthibitisha kuwa muhtasari huo upo sahihi, hivyo kuruhusu usainiwe kwa ajili ya kumbukumbu za Halmashauri. Aidha, Sekretarieti iliwasilisha majibu yatokanayo na kikao hicho kisha majibu ya utekelezaji yalipokelewa na kikao kuelekeza kuwa:-

1. ***Mweka Hazina (W) atoe taarifa juu ya utengaji wa fedha asilimia kumi (10%) ya makusanyo ya ndani kila mwezi kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu. Taarifa hiyo ionyeshe ni fedha kiasi gani zimekusanywa kwa mwezi husika na asilimia kumi (10%) ya hizo fedha itengwe kisha kuhamishiwa kwenye akaunti maalum ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.***

2. ***Vituo vya kutolea huduma za Afya ambavyo vimekuwa na makusanyo hafifu sana Mkaguzi wa ndani kwa kushirikiana na Mfamasia, afanye Ukaguzi maalumu ili kubaini sababu zinazopelekea hali hiyo. Mara ukaguzi huo utakapokamilika taarifa iwasilishwe.***

## CMT/KOG/2021-22/05/04: KUSOMA NA KUPITIA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA CHA TAREHE 09 FEBRUARI, 2022 NA KUPITIA YATOKANAYO NA KIKAO HICHO.

Menejimenti ilipitia muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha cha tarehe 09/02/2022 kisha kufanya masahihisho na kuelekeza muhtasari huo uandaliwe kwa ajili ya kabrasha la kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 28/02/2022.

## CMT/KOG/2020-21/04/05. TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI

### A. MAPATO YA NA MATUMIZI YA HALMASHAURI KWA MWEZI JANUARI, 2022

- **MAPATO**

Katika kipindi cha mwezi unaoishia tarehe 31 Januari, 2022 Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ilipokea fedha Jumla ya Tshs 2,925,522,909.40 kutokana na vyanzo mbalimbali sawa na 86.6 % ya makisio ya mwezi ya Jumla ya Tshs 3,378,905,981.42. Kati ya fedha hizi, Tshs 224,781,867.50 sawa na 84.10% ya lengo la Tshs 267,290,625 kwa mwezi zimetokana na vyanzo vya ndani vya Halmashauri na Tshs 2,139,672,700 sawa na 101.40% ya lengo la Tshs 2,109,689,814.75 ni ruzuku toka Serikali kuu kwa ajili ya kulipia Mishahara. Kwa upande wa matumizi ya kawaida (OC) Halmashauri ilipokea kiasi cha Tshs 26,991,916.70 ambayo ni sawa na 21.30% ya lengo la Tshs 126,595,250.0 kwa mwezi.

Aidha kutoka Kwa Wahisani mbalimbali na Serikali Kuu, zilipokelewa Tshs 534,076,425.20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na 61% ya makisio ya Tshs 875,330,291.67 kwa mwezi.

- **MATUMIZI:**

Jumla ya Tshs 3,460,248,009.90 zilitumika katika kipindi cha kuishia tarehe 31 mwezi Januari, 2022 Kwa ajili ya kulipia mishahara, miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo sawa na 102.40 % ya makisio ya jumla ya Tshs 3,378,905,981.42 kwa mwezi. Kati ya matumizi haya Tshs



Scanned with CamScanner

409,290,653.80 sawa na 153.13% ya lengo la Tshs 267,290,625 zimetokana na vyanzo vya ndani vya Halmashauri. Aidha kiasi cha Tshs 2,139,672,700 sawa na 101.40 % ya lengo la Tshs 2,109,689,814.75 ni ruzuku ya mishahara. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya kawaida (OC)

Halmashauri ilitumia kiasi cha Tshs 26,346,000 ambayo ni sawa na 20.8% ya makisio ya Tshs 126,595,250.00 kwa mwezi. Kwa upande wa miradi ya maendeleo Halmashauri ilitumia kiasi cha Tshs 884,938,656.10 ambayo ni sawa na 101.10 % ya jumla ya makisio ya Tshs 875,330,291.7 kwa mwezi.

Mchanganuo wa muhtasari wa mapato na matumizi haya ni kama unavyoonekana katika jedwali linalofuata:-

**MAPATO NA MATUMIZI MWEZI JANUARI 2022**

| Na | Kasma Ya Mapato | A: Bajeti ya Mwezi Januari 2022 (Tshs) | B: Mapato Halisi Mwezi Januari 2022 (Tshs) | C: Matumizi halisi mwezi Januari 2022 (Tshs) | D: Pungufu/Ziada (Tshs) (B-C) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya ndani ya Halmashauri **(Bila lindwa)** | 184,064,875 | 141,542,387.13 | 357,080,237.10 | (215,537,849.97) |
| 2 | Mapato ya ndani ya Halmashauri **(Lindwa)** | 83,225,750 | 83,239,480.40 | 52,210,416.70 | 31,029,063.70 |
| | **Jumla Ndogo Mapato ya Ndani** | **267,290,625** | **224,781,867.53** | **409,290,653.80** | **(184,508,786.27)** |
| 3 | Ruzuku ya Kawaida (Mishahara) | 2,109,689,814.8 | 2,139,672,700 | 2,139,672,700 | 0 |
| 4 | Ruzuku ya matumizi Mengine (o.c) | 126,595,250 | 26,991,916.70 | 26,346,000 | 635,916.70 |
| 5 | Miradi ya Maendeleo | 875,330,291.7 | 534,076,425.20 | 884,938,656.10 | (350,862,230.90) |
| | ***Jumla Ndogo Ruzuku*** | **3,111,615,356.5** | **2,700,741,041.90** | **3,050,957,356.10** | **(350,226,314.20)** |
| | **JUMLA KUU** | **3,378,905,981.4** | **2,925,522,909.43** | **3,460,248,009.90** | **(534,735,100.47)** |

**Maelezo ya jedwali ni kama ifuatavyo:**

- Fedha za mishahara zimetumika kama zilivyopokelewa.
- Fedha za ruzuku ya matumizi Mengineyo (o.c) zimetumika kidogo kwa sababu fedha zilizoingia mwezi Januari hazikutumika zote na matumizi yake yataonekana mwezi Februari 2022.
- Fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri zimetumika zaidi ya zilizokusanywa kwa sababu fedha zilizohamishwa kutoka akaunti ya makusanyo kwenda akaunti ya maendeleo miezi ya nyuma zilitumika mwezi Januari 2022 kukamilisha Ujenzi wa Zahanati na Shule mpya za Sekondari.
- Fedha za miradi ya maendeleo za Mfuko wa Jimbo, Mfuko wa pamoja wa Afya (Basket fund) na TASAF zilizoingia mwezi Disemba 2021 zilitumika Januari 2022



Scanned with CamScanner

**Taarifa ilipokelewa kisha wajumbe kushauri na kuazimia yafuatayo:-**

*i)* *Ofisi ya Mweka Hazina kupitia jopo la ukusanyaji na ufuatiliaji wa mapato ya Halmashauri iweke mikakati ya kuongeza mapato hususani katika vyanzo lindwa.*

*ii)* *Maeneo ambayo hayana POS ilhali yanahitaji mashine hizo, kikao kilishauri kuwa POS zipatikane ili zitumike katika maeneo hayo kwa minajili ya kuongeza mapato ya Halmashauri.*

***iii)*** ***Azimio:*** ***Kwa kuwa Halmashauri ilikwishatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa mashine mpya za POS, iliazimiwa kuwa Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi aeleze ni hatua gani zimefikiwa ili kupatikana kwa mashine hizo.***

*iv)* *Maeneo yenye POS ilhali makusanyo katika maeneo hayo ni kidogo, Idara ya Fedha na Biashara ione kama kuna uwezekano wa kuhamishia POS hizo/hiyo kwenye maeneo ambayo makusanyo yake ni makubwa pindi Halmashauri ikiendelea kutatua changamoto ya uchache wa mashine za kukusanyia mapato.*

## B. MAPATO NA MATUMIZI KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA KWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANAURI, 2022 KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Idara ya Afya ina jumla ya vituo vya kutolea huduma za Afya 62 vinavyowasilisha taarifa za mapato na matumizi kila mwezi katika Halmashauri.

### MAPATO

Vyanzo vikuu vya mapato katika idara ya Afya katika kipindi cha Januari, 2022 vilihusisha:-

1) Mfuko wa Afya ya jamii (CHF),
2) Mfuko wa pamoja wa Afya (HSBF),
3) Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF),
4) Malipo ya Papo kwa papo (User fee),
5) Central Government grants,
6) Drug revolving fund (DRF)

### SALIO ANZIA NA MAKUSANYO KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2022

Salio anzia kwa mwezi Januari, 2022 lilikuwa Tsh. **1,614,977,284.77**

Katika kipindi cha Januari, 2022, Idara ya Afya imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Tshs. 85,832,205.17** ambapo kiasi cha Tsh. 85,672,830.26 ni mapato ya ndani (User Fee, CHF, NHIF na DRF) na kiasi cha **Tsh. 159,374.91** ni fedha za UVIKO19, kwa mchanganuo ufuatao:



Scanned with CamScanner

| JINA LA KITUO | MAPATO | | | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | USER FEE (B) | NHIF | CHF (D) | DRUG REVOLVING FUND (DRF) | UVIKO-19 | |
| HOSPITALI YA WILAYA | 6,753,600.00 | 29,777,595.00 | 1,274,307.53 | 6,350,900.00 | - | 44,156,402.53 |
| VITUO VYA AFYA | 12,980,650.00 | 10,280,335.02 | 3,465,173.15 | - | - | 26,726,158.17 |
| ZAHANATI | 4,272,000.00 | 2,707,830.00 | 7,810,439.56 | - | 159,374.91 | 14,949,644.47 |
| **JUMLA** | **24,006,250.00** | **42,765,760.02** | **12,549,920.24** | **6,350,900.00** | **159,374.91** | **85,832,205.17** |

Jumla ya fedha zote (Salio anzia + Makusanyo) = **Tsh. 1,700,809,489.94.**

## MATUMIZI

Katika kipindi cha Januari, 2022, Idara ya Afya ilifanya matumizi katika vituo vya kutolea huduma za Afya jumla ya **Tshs. 606,155,045.03** kwa mchanganuo ufuatao:-

| KITUO | MATUMIZI |
|---|---|
| HOSPITALI YA WILAYA | 201,644,453.20 |
| VITUO VYA AFYA | 185,749,543.03 |
| ZAHANATI | 218,761,048.80 |
| **JUMLA** | **606,155,045.03** |

Aidha baada ya matumizi kwa kipindi cha Janauari, 2022 salio bakia ni jumla ya **Tshs. 1,094,954,444.88**

## CHANGAMOTO

i) Baadhi ya vituo kukosa wateja wanaopata huduma kupitia mfuko wa Bima ya afya (NHIF).

ii) Ucheleweshaji wa malipo ya bima ya CHF

## HATUA ZILIZOCHUKULIWA;

i) Wilaya imefanikiwa kufanya mazungumzo na benki ya NMB kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa mapato moja kwa moja kutoka kwa wagonjwa/wateja. Aidha, Wakala wa makusanyo ngazi ya Hospitali amepatikana na tayari benki wamempatia mkataba kwa ajili ya kutoa huduma hiyo. Mchakato wa kutafuta mawakala katika ngazi ya vituo vingine unaendelea kuratibiwa na benki ya NMB.

ii) Kuhimiza vituo kutoa huduma kupitia Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF).

iii) Kuhimiza watumishi kutuma madai ya bima za NHIF na CHF kwa wakati. **Taarifa ilipokelewa.**



Scanned with CamScanner

## CMT/KOG/2021-22/05/06. TAARIFA YA MAKUSANYO YA MFUKO WA ELIMU KWA MWEZI JANUARI, 2022 KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa imekuwa na Mfuko wa Elimu kwa ajili ya kutatua changamoto za Elimu katika kata husika, ambapo kila mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi (miaka 18-60) anatakiwa kuchangia Tsh 10,000 kwa mwaka. Idadi ya nguvu kazi katika Halmsahauri ya Wilaya ya Kongwa inakadiriwa kuwa ni 93,740 hivyo lengo ni kukusanya Tsh 930,740,000. Na kwa mwezi Januari jumla ya Tsh **781,000.00** zimekusanywa na kufanya jumla ya makusanyo kutoka Julai- Januari kuwa **243,433,776** sawa na 26.15 %. Mchanganuo wa makusanyo na matumizi kwa kila kata umeainishwa katika jedwali

**Taarifa ya makusanyo na Matumizi kwa kila Kata**

| NA | KATA | LENGO KWA MWAKA 2021/2022 | MAKUSANYO JAN, 2022 | SALIO DES+ MAPATO YA JAN, 2022 | MATUMIZI JAN, 2022 | SALIO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KONGWA | 40,630,000.00 | 190,000.00 | 3,028,000.00 | | 3,028,000.00 |
| 2 | CHAMKOROMA | 44,060,000.00 | - | 304,000.00 | | 304,000.00 |
| 3 | CHITEGO | 29,420,000.00 | - | 428,600.00 | | 428,600.00 |
| 4 | CHIWE | 58,490,000.00 | - | 12,260,000.00 | | 12,260,000.00 |
| 5 | HOGORO | 51,430,000.00 | - | 9,372,900.00 | | 9,372,900.00 |
| 6 | IDUO | 33,620,000.00 | - | 12,720,000.00 | | 12,720,000.00 |
| 7 | KIBAIGWA | 74,350,000.00 | - | 205,000.00 | | 205,000.00 |
| 8 | LENJULU | 43,360,000.00 | - | 488,000.00 | | 488,000.00 |
| 9 | MAKAWA | 25,890,000.00 | - | 15,490,000.00 | | 15,490,000.00 |
| 10 | MATONGORO | 30,310,000.00 | - | 10,956,000.00 | | 10,956,000.00 |
| 11 | MKOKA | 35,810,000.00 | - | 13,520,000.00 | | 13,520,000.00 |
| 12 | MLALI | 58,920,000.00 | - | 3,350,000.00 | | 3,350,000.00 |
| 13 | MTANANA | 37,710,000.00 | - | 1,777,163.00 | | 1,777,163.00 |
| 14 | NGHUMBI | 34,560,000.00 | 20,000.00 | 568,000.00 | | 568,000.00 |
| 15 | NGOMAI | 31,630,000.00 | - | 9,920,000.00 | | 9,920,000.00 |
| 16 | NJOGE | 30,220,000.00 | 571,000.00 | 6,622,800.00 | | 6,622,800.00 |
| 17 | PANDAMBILI | 24,030,000.00 | - | 1,040,000.00 | | 1,040,000.00 |
| 18 | SAGARA | 66,260,000.00 | | 1,050,000.00 | | 1,050,000.00 |
| 19 | SEJELI | 57,340,000.00 | - | 651,500.00 | | 651,500.00 |
| 20 | SONGAMBELE | 53,180,000.00 | | 14,630,000.00 | | 14,630,000.00 |
| 21 | UGOGONI | 51,190,000.00 | - | 2,613,000.00 | | 2,613,000.00 |
| 22 | ZOISSA | 18,330,000.00 | - | 2,204,976.00 | | 2,204,976.00 |
| | **JUMLA** | **930,740,000.00** | **781,000.00** | **123,199,939.00** | **0.00** | **123,199,939.00** |

**Taarifa ilipokelewa**

## CMT/KOG/2021-22/05/07. HOJA YA UENDESHAJI WA MACHINJIO YA KUKU, KIWANDA CHA MAZIWA NA BWAWA LA UFUGAJI WA SAMAKI

Kikao kilielezwa kuwa, lengo la Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo Halmashauri za Majiji, Wilaya na Miji ni kutoa huduma za kijamii na kiuchumi kwa wakazi wake. Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni elimu, afya, maji, miundombinu nk. Halmashauri pia hutoa leseni za kuendesha shughuli mbalimbali za kibiashara kwa wakazi wake. Kwa mantiki hiyo, Mamlaka za



Scanned with CamScanner

Serikali za Mitaa hazifanyi biashara ya moja kwa moja. Hata hivyo, inapendekezwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na miradi ya kiuchumi ili kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato. Changamoto kubwa ni usimamizi na uendelevu wa miradi hiyo.

Kwa sekta ya Mifugo na Uvuvi, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina miradi ya kibiashara na huduma kama vile:

- Majosho ya kuogeshea mifugo, kituo cha unenepeshaji mifugo,
- Mapakilio, minada na magulio ya mifugo, kiwanda cha kusindika maziwa,
- Machinjio za ng'ombe/Mbuzi na kuku, bwawa la ufugaji samaki.

Uendeshaji na usimamizi wa miradi hii unahitaji mfumo imara unaowajibika kuhakikisha kuwa miradi hiyo inajiendesha kibiashara (inarejesha gharama za uwekezaji, uendeshaji na kuzalisha faida) na inakuwa endelevu. Ili kufikia mafanikio bora katika miradi ya machinjio ya kuku, kiwanda cha maziwa na bwawa la ufugaji samaki. Inaipasa Halmashauri kuiendesha kwa mfumo shirikishi wa kujenga pangisha (Public Private Partinership-PPP).

Aidha, Muundo wa PPP utahusisha Serikali kutoa miundombinu na sekta binafsi kwa ajili ya kutoa fedha za uendeshaji, magari ya barafu kwa ajili ya kusafirishia bidhaa na ukarabati wa miundombinu. Ni vema kazi ya kuunda na kuendesha mfumo shirikishi wa PPP ikafuata matakwa ya kisheria na kubainisha mgawanyo wa faida kwa pande zote mbili. Moja ya faida za kutumia PPP ni kupunguza gharama za uendeshaji kwa serikali na kuongeza usimamizi wa kibiashara kwa miradi.
Wajumbe wa Menejimenti waliombwa kutoa ushauri/uamuzi wa kutumia mfumo wa PPP kwa ajili ya uendeshaji wa miradi ya machinjio ya kuku, kiwanda cha maziwa na bwawa la samaki -Tubugwe kiufanisi na kuhakikisha uendelevu wa miradi hiyo.

Tarifa ilipokelewa kisha wajumbe kuridhia hoja hiyo na kuelekeza kuwa iwasilishwe kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa ajili ya maamuzi zaidi.

## CMT/KOG/2021-22/05/08.TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UVIKO-19 KWA IDARA ZA AFYA, ELIMU MSINGI NA SEKONDARI.

### I. IDARA YA AFYA.

Mkuu wa Idara ya Afya aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya UVIKO-19 akieleza kuwa Idara ya Afya ilipokea kiasi cha Tsh 300,000,000/= milioni mia tatu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura na tarehe 04/02/2022 fedha kiasi cha Tsh 90,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in 1) kilipokelewa katika kituo cha Afya Sejeli. Aidha alieleza kuwa ujenzi wa nyumba ya watumishi tayari imekwisha anza kuanzia tarehe 11/02/2022 na tarehe 07/02/2022 kazi ya ujenzi wa jengo la dharura (EMD) ilianza huku akieleza kuwa ujenzi wa majengo hayo unaendelea vizuri.



Scanned with CamScanner

### II. IDARA YA ELIMU MSINGI.

Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19 huku akieleza utekelezaji huo kuwa ni kukamilisha ujenzi wa shule shikizi 07 zenye madarasa 18 na ujenzi wa bweni moja kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule ya msingi Mkoka (Tazama kiambatisho A).

### III. IDARA YA ELIMU SEKONDARI.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19 huku akieleza utekelezaji huo kuwa ni kukamilisha ujenzi wa madarasa 112. (Tazama kiambatisho A).

## CMT/KOG/2021-22/05/09. KUFUNGA KIKAO

Katibu wa kikao alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa michango yao katika kujadili ajenda zote zilizowasilishwa, ambapo pamoja na masuala mengine ya kiutendaji, wajumbe walisisitizwa kuandaa vizuri taarifa ambazo zinapaswa kuwasilishwa katika kikao cha kamati ya Fedha. Baada ya msisitizo huo, Mwenyekiti alifunga kikao saa 7:40 mchana.

**UMETHIBITISHWA**

MWENYEKITI

17/03/2022

TAREHE

KATIBU



Scanned with CamScanner

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA MENEJIMENTI CHA TAREHE 24 FEBRUARI, 2022

| NA | AZIMIO/AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | ***Iliazimiwa kuwa, Mweka Hazina (W) awe anatoa taarifa juu utengaji wa fedha asilimia kumi (10%) ya makusanyo ya ndani kila mwezi kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Walemavu. Taarifa hiyo ionyeshe ni fedha kiasi gani zimekusanywa kwa mwezi husika na 10% ya hizo itengwe kisha kuhamishiwa kwenye akaunti maalum ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.*** | DT | *Agizo limezingatiwa.*<br><br>Makusanyo ghafi (bila lindwa) kwa mwezi Februari, 2022 ni **Tshs. 124,268,803.70** Asilimia 10 ya fedha hizo ni **Tshs. 12,426,880.37** na ndicho kiasi kilichotengwa na kuwekwa kwenye akaunti maalumu ya vikundi vya wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu. |
| 2. | ***Kikao kiliazimia kuwa vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vimekuwa na makusanyo hafifu sana Mkaguzi wa ndani kwa kushirikiana na Mfamasia afanye Ukaguzi maalumu ili kubaini sababu zinazopelekea hali hiyo. Taarifa ya utekelezaji iwasilishwe.*** | DIA | |
| 3. | ***Kwa kuwa Halmashauri ilikwishatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa mashine mpya za POS, iliazimiwa kuwa Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi aeleze ni hatua gani zimefikiwa ili kupatikana kwa mashine hizo.*** | HPMU | |



Scanned with CamScanner

KIAMBATISHO A.

# TAARIFA YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 130 (SHULE ZA SEKONDARI (112) NA MSINGI -SHIKIZI 07 ZENYE MADARASA 18) PAMOJA NA UJENZI WA BWENI MOJA KATIKA SHULE YA WANAFUNZI WA WENYE MAHITAJI MAALUMU.

## 1.0 UTANGULIZI

**Ndugu Mwenyekiti**, Kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko-19 katika sekta ya Elimu, Wilaya imepokea kiasi cha fedha Tshs 2, 680, 000,000 kwa ajili Ujenzi wa madarasa 130 (112 ya Sekondari na 18 ya shule za Msingi) pamoja na bweni moja la wanafunzi wa elimu maalum.

Wilaya ilijipanga kikamilifu kuhakikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa unakamilika kabla ya mwisho wa mwezi Desemba, 2021 ili wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka 2022 waweze kusomea katika madarasa haya. Aidha ili kupunguza msongamano wa wanafunzi shuleni na kupunguza umbali wa wanafunzi kutembea hadi shuleni, Uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na Mhe. Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliazimia kuanzisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika maeneo yenye umbali mrefu ili kupunguza mwendo kwa wanafunzi pamoja na kuendeleza shule mpya katika kata ya Chitego. Jumla ya shule mpya saba (7) katika kata za Kongwa, Chamkoroma, Chiwe, Njoge, Kibaigwa, Sejeli na Chitego.

### 1.1 Utekelezaji wa Miundombinu

Utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya Vyumba vya madarasa kwa shule za msingi na sekondari umekamilika kwa asilimia mia moja. Aidha kwa upande wa utengenezaji wa samani (viti,meza na madawati ) kwa shule za Sekondari na msingi upo hatua za mwisho za ukamilishaji. Wilaya imetumia mikakati mbalimbali kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati. Mikakati hii ni pamoja na;

- Vifaa vya ujenzi kununuliwa kwa pamoja (Bulky Procurement) na majengo kujengwa kwa kutumia force akaunti.
- Kamati za ujenzi za shule kuundwa na kujengewa uwezo wa namna ya kujenga miundombinu hii kwa kutumia force akunti
- Halmashauri ilifanya kikao cha pamoja kwa kamati za ujenzi, viongozi wa kata (Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, watendaji wa kata na Vijiji) kwa ajili ya kuwapa maelekezo na taratibu za namna ya kusimamia ujenzi.
- Kuhamsisha Jamii na kushirikisha wadau wengine wa maendeleo kuchangia nguvu kazi ili ujenzi ukamilike kwa wakati.
- Ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa kila hatua ya ujenzi.



Scanned with CamScanner

- Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliunda timu maalum ya ufuatiliaji.

Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa kwa kila shule na idadi ya Miundombinu iliyojengwa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

| Na | Jina La Mradi | Jina La Kituo/Shule | Idadi ya Miundombinu | Kiasi idhinishwa | Kiasi Kilichotolewa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 7 Shule za Sekondari | MANG'HAILA | 7 | 140,000,000 | 140,000,000 |
| 2 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 3 Shule za Sekondari | MUMI | 3 | 60,000,000 | 60,000,000 |
| 3 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 3 Shule za Sekondari | IBWAGA | 3 | 60,000,000 | 60,000,000 |
| 4 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | SONGAMBELE | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |
| 5 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | SEJELI | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |
| 6 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | SAGARA | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |
| 7 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | LAIKALA | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |
| 8 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 6 Shule za Sekondari | PANDAMBILI | 6 | 120,000,000 | 120,000,000 |
| 9 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 3 Shule za Sekondari | HEMBAHEMBA | 3 | 60,000,000 | 60,000,000 |
| 10 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | NGOMAI | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |
| 11 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | NGHUMBI | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |
| 12 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 3 Shule za Sekondari | NDALIBO | 3 | 60,000,000 | 60,000,000 |
| 13 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | MTANANA | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |
| 14 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | MLALI | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |
| 15 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 5 Shule za Sekondari | ZOISSA | 5 | 100,000,000 | 100,000,000 |
| 16 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 3 Shule za Sekondari | NORINI | 3 | 60,000,000 | 60,000,000 |
| 17 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 5 Shule za Sekondari | MAKAWA | 5 | 100,000,000 | 100,000,000 |
| 18 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 2 Shule za Sekondari | MNYAKONGO | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 |
| 19 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 2 Shule za Sekondari | KONGWA | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 |
| 20 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 5 Shule za Sekondari | NDURUGUMI | 5 | 100,000,000 | 100,000,000 |
| 21 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 6 Shule za Sekondari | KIBAIGWA | 6 | 120,000,000 | 120,000,000 |
| 22 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 4 Shule za Sekondari | IDUO | 4 | 80,000,000 | 80,000,000 |



Scanned with CamScanner

| Na | Jina La Mradi | Jina La Kituo/Shule | Idadi ya Miundombinu | Kiasi idhinishwa | Kiasi Kilichotolewa |
|---|---|---|---|---|---|
| 23 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 5 Shule za Sekondari | HOGORO | 5 | 100,000,000 | 100,000,000 |
| 24 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 6 Shule za Sekondari | BANYIBANYI | 6 | 120,000,000 | 120,000,000 |
| 25 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 6 Shule za Sekondari | CHIWE | 6 | 120,000,000 | 120,000,000 |
| 26 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 6 Shule za Sekondari | MANG,HWETA | 6 | 120,000,000 | 120,000,000 |
| 27 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwenye vituo Shikizi vya Shule za Msingi | CHITEGO S/M (MATULI KITUO SHIKIZI) | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 |
| 28 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwenye vituo Shikizi vya Shule za Msingi | KITETO S/M (KONYEKI KITUO SHIKIZI) | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 |
| 29 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwenye vituo Shikizi vya Shule za Msingi | MAJAWANGA S/M (MLIMANI KITUO SHIKIZI) | 3 | 60,000,000 | 60,000,000 |
| 30 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwenye vituo Shikizi vya Shule za Msingi | MLANJE S/M (WEZAMTIMA KITUO SHIKIZI) | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 |
| 31 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwenye vituo Shikizi vya Shule za Msingi | MSUNJILILE S/M (NJIDA KITUO SHIKIZI) | 5 | 100,000,000 | 100,000,000 |
| 32 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwenye vituo Shikizi vya Shule za Msingi | NDACHI S/M (NGH'OLE KITUO SHIKIZI) | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 |
| 33 | Ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwenye vituo Shikizi vya Shule za Msingi | SEJELI S/M (MUUNGANO KITUO SHIKIZI) | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 |
| 34 | Ujenzi wa Bweni kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu | SHULE YA MSINGI MKOKA | 1 | 80,000,000 | 80,000,000 |

**1.2 Changamoto katika utekelezaji**

Katika kutekeleza ujenzi wa miundombinu hii, halmashauri imekumbana na changamoto zifuatazo;

Katika kutekeleza ujenzi wa miundombinu hii, halmashauri imekumbana na changamoto zifuatazo; kwa kiwango kikubwa.

i. Kupanda kwa bei kwa baadhi ya vifaa vya ujenzi kwa kiwango kikubwa.

ii. Ukosefu wa maji kwa baadhi ya maeneo ya mradi, hali iliyosababisha tofali kufyatuliwa umbali zaidi Km 25 kutoka eneo la mradi Mfano kata ya Njoge tofali zake zilifyatuliwa kata ya Pandambili.

iii. Baadhi ya Wanachi kutokua tayari kuchangia nguvu kazi katika ujenzi wa madarasa.

iv. Kukatika kwa umeme mara kwa mara hasa kwa wazalishaji wa tofali (wazalishaji wanao tumia mashine za umeme) na mafundi wa kutengeneza madirisha na samani.



Scanned with CamScanner

### 1.3 Utatuzi wa Changamoto

Katika kukabiliana na hizo changamoto,Halmashauri ya wilaya ilichukua hatua za makusudi za;

i. Kuagiza vifaa vya ujenzi kutoka kiwandani ambako bei ni rafiki na kusaidia kupunguza gharama ambazo zingeweza kuongezeka endapo vingenunuliwa kwa wazabuni wa ndani.

ii. Uongozi wa wilaya ulishirikiana na wataalamu wa Idara ya maji na kuhakikisha shule zilizokuwa na uhaba wa maji zinaunganishiwa mfumo wa maji na kufungulia maji kuelekeza maeneo ya ujenzi. Aidha kwa shule zisizo na vyanzo vya maji jitihada ya kuweka matenki makubwa ya maji zilifanyika ili kuhakikisha maji ya kutosha yanapatikana muda wote wa utekelezaji wa mradi.

**Mwisho;**

Pamoja na Changomoto zote tulizokumbana nazo katika kuteleza zoezi hili, leo tunayo furaha kukukabidhi vyumba 130 vya madarasa (Sekondari 112 na Msingi – shule shikizi 18). Aidha nashukuru sana kwa ushirikiano tulioupata kutoka kwa Viongozi ngazi ya Vijiji, kata na wilaya. Wewe binafsi na kamati yako ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, waheshimiwa Madiwani, Viongozi wa Chama Tawala, Wanachi pamoja na walimu na watumishi wengine wote.

Kwa heshima na taadhima sasa naomba nikukabidhi vyumba 130 vya madarasa (Sekondari 112 na Msingi – shule shikizi 18).

**Nawasilisha ,**



Scanned with CamScanner